
COMPETENCE BASED CURRICULUM
HOMEWORK ENGAGEMENT PROGRAM
GREDI 5 2024 AGOSTI
KISWAHILI

KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu swali la 1 hadi la 5

(Ni asubuhi baada ya gwaride. Kasim anabisha mlango wa ofisi ya Mwalimu Mkuu. Mwalimu anamkaribisha ndani.)



Kasim : (Akiinama kwa heshima.) Shikamoo mwalimu?

Mwalimu mkuu : Marahaba Kasim. Umeamkaje? Natumai kila kitu ni salama. Si kawaida yako kunitembelea ofisini asubuhi.

Kasim : Nimeamka vyema mwalimu. Nashukuru. Hakika niliamka alfajiri. Mzazi wangu aliniamsha ili anikabidhi barua hii. *(Anamkabidhi mwalimu bahasha.)*

Mwalimu mkuu : Aha! Nilijua lazima una sababu ya kuja ofisini mwangu asubuhi. Barua ina ujumbe gani?

Kasim : Sina habari. Nimepewa tu. Labda ni mwaliko au jambo fulani. Mwalimu, ulitufunza kuwa si vyema kusoma barua za watu wengine.

Mwalimu mkuu : (Akimpongeza.) Hongera Kasim. Wewe ni mtoto mwema. Ni vizuri kutosoma barua ambazo si zako.

Kasim : (Akinyenyekea.) Shukran mwalimu. Mzazi wangu pia **hunihimiza** niwe na uaminifu kwa kuwa, heshima si utumwa.

Mwalimu mkuu : Nashukuru kwa maneno yako. Sasa unaweza kujiunga na wengine darasani. Endelea kutia bidii za mchwa masomoni. Nitakupatia majibu ya barua alasiri.

Kasim : Asante mwalimu. Kwaheri. Tutaonana wakati huo wa alasiri.

Mwalimu mkuu : Kwaheri ya kuonana.

1. Je, Kasim alienda katika ofisi ya mwalimu wakati gani?
    A. Jioni
    B. Alasiri
    C. Adhuhuri
    D. Asubuhi
2. Kitendo cha Kasim kutoisoma barua aliyopewa na mama yake kinaonyesha maadili gani?